Habarileo Jumamosi Aprili 4, 2026

# Latra yapiga marufuku migomo kwa wasafirishaji

Na Ikunda Erick

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imepiga marufuku migomo kwa watoa huduma za usafirishaji na kusisitiza kuwa haitamvumilia yeyote atakayekiuka utaratibu wa kisheria katika kupanga nauli, huku ikiwataka wadau kufuata mifumo rasmi iliyowekwa.

Mkurugenzi Mkuu wa Latra, Habibu Suluo alisema hayo Dar es Salaam juzi baada ya baadhi ya madereva mkoani Mbeya kugoma kutoa huduma za usafiri, kwa madai kuwa kupanda kwa bei ya mafuta hakuendani na nauli zilizopo.

"Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya waendesha mabasi kuhusu kupanda kwa gharama za uendeshaji, ikiwemo bei ya mafuta lakini hilo haliwezi kuwa sababu ya kufanya mgomo au kuongeza nauli kiholela," alisema Suluo.

Alisema kuna kikokotoo maalumu kinachotumika kupanga nauli kwa kuzingatia gharama halisi za uendeshaji na kwamba kwa sasa hesabu zinaonesha waendeshaji wanaweza kuendelea kutoa huduma bila kupata hasara, hata katika hali ya sasa ya bei za mafuta.

"Yeyote atakayesitisha huduma au kushiriki mgomo kinyume cha sheria, hatua kali zitachukuliwa ikiwemo kufungiwa leseni," alisema.

Aidha, alisema baadhi ya changamoto zinazotajwa na waendeshaji zinatokana na mifumo isiyo rasmi ya ukusanyaji wa mapato ambapo wamiliki wa mabasi wanashindwa kufuatilia mapato halisi yanayopatikana kila siku.

Mamlaka imeonya kuwa ipo tayari kuanzisha mfumo wa tiketi za mtandaoni kwa mabasi yote ili kuweka uwazi wa mapato na kuondoa malalamiko yasiyo na msingi.

"Iwapo watoa huduma hawatakuwa tayari kuweka mifumo ya uwazi, serikali inaweza kuwalazimisha kutumia tiketi za kielektroniki ili kila mmiliki aweze kuona mapato yanayoingia kwa wakati halisi," alisema.

Pia, imewataka wamiliki wa mabasi kuwasilisha takwimu sahihi za uendeshaji ili kusaidia kufanya maamuzi ya haki kuhusu nauli, ikisisitiza kuwa maamuzi yoyote lazima yazingatie sheria na taratibu zilizopo.

Kwa upande mwingine, Latra imesisitiza kuwa milango ya majadiliano ipo wazi kwa wadau wote wa sekta hiyo na imewataka kujitokeza kwa mazungumzo badala ya kuchukua hatua zisizo halali.

Aidha, alitoa mwito kwa wadau wote wa usafirishaji kuhudhuria kikao kilichoitishwa Aprili 8, mwaka huu mjini Dar es Salaam kuwasilisha maoni na mapendekezo yao kuhusu nauli kwa kuzingatia kanuni na vigezo.

Alitaja baadhi ya vigezo hivyo kuwa, wadau lazima wawasilishe hesabu zao zilizokaguliwa kwa miaka mitatu mfululizo, wawasilishe taarifa ya utendaji wa kampuni kwa miaka mitano mfululizo na wawasilishe taarifa ya mishahara inayolipwa kwa dereva na kondakta.

Alisema wadau watakaoshindwa kufika ana kwa ana Dar es Salaam wanaweza kushiriki mkutano huo moja kwa moja kupitia mitandao ya Latra itakayorushwa moja kwa moja wakati wa kikao hicho.

CamScanner